Sustainable Development Verified Impact Standard

MRADI WA KASIGAU CORRIDOR REDD+
AWAMU YA II-COMMUNITY RANCHES (KCRPII)

Imetayarishwa na Wildlife Works Carbon LLC.



Mradi wa Kasigau REDD+ Awamu ya II – Community Ranches (KCRPII) iko Kusini Mashariki mwa Kenya katika Mkoa wa Pwani mwendo wa masaa mawili ukitumia gari kutoka mji wa bandari wa Mombasa. Eneo la mradi linaunganishwa na mazingira ya misitu iliyo kavu, inayotawaliwa na speshi kama vile akacia na komiphora na aina nyingine zinazostahimili ukame. Idadi kubwa ya watu katika eneo hilo wanatoka katika kabila la wataita, wengine wanao ishi katika maeneo hayo ni waduruma, wakamba na makabila mengine kutoka pande zote za nchi.

Mradi wa Ujenzi wa Wanyamapori wa Kasigau REDD+ umegawanywa katika Awamu mbili, Awamu ya I - Rukinga Sanctuary na Awamu ya II – Community Ranches. Ingawa miradi yote miwili imesajiliwa kibinafsi kama miradi ya kipekee chini ya Viwango vya VCS & CCB vya Mpango wa Verra, inasimamiwa ipasavyo kama mradi mmoja mashinani na katika ngazi ya usimamizi.

Hati hii ya Maelezo ya Mradi (PD) inashughulikia KCRPII ya mradi na inashughulikia uhifadhi wa misitu ya vitalu 13 vya ardhi vinavyomilikiwa na Vikundi vya Umiliki wa Jamii za Wenyeji. Kila moja ya vitalu kumi na tatu vikimilikiwa na mashirika tofauti ya kisheria yaliyoundwa miaka iliyopita na Jumuiya na Serikali ya Kenya ili kumiliki hatimiliki ya ardhi hiyo.

Vitalu 13 vya ardhi vilivyofunikwa chini ya Awamu hii ya Pili ya Mradi wa MKUHUMI wa Kasigau Corridor vina jumla ya hekta 169,741 na ni:

- Taita Ranch: hekta 35,612 pia inajulikana kama LR 12264 inayomilikiwa na Taita Ranching Company Ltd mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Mgeno Ranch: hekta 21,232 pia inajulikana kamaLR 12178 inayomilikiwa na Mgeno Ranching (DA) Company Ltd mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Maungu Ranch: hekta 21,619 ha pia inajulikana kama LR 12179, inayomilikiwa na Maungu Ranching (DA) Company Ltd. mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Kasigau Ranch: hekta 21,186 pia inajulikana kama LR 12180, inayomilikiwa na Kasigau Ranching (DA) Company Ltd., mkusanyiko wa wanahisa wazawa..
- Wangala Ranch: hekta 2,023.5 pia inajulikana kama LR 12262 inayomilikiwa na Livingstone and Alphonce Ikonge, mkusanyiko wa wanahisa wazawa..
- Kambanga Ranch: hekta12,948 pia inajulikana kama FR 195/6 inayomilikiwa na Kasigau Ranching (DA) Company Ltd., mkusanyiko wa wanahisa wazawa..
- Dawida Ranch: hekta 4,046.86 pia inajulikana kama LR 14208 inayomilikiwa na Dawida Ranching Group Company Ltd., mkusanyiko wa wanahisa wazawa..
- Washumbu Ranch: hekta 14,501 pia inajulikana kama LR 14206 inayomilikiwa na Washumbu (DA) Ranching Company Ltd., mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Amaka Ranch: hekta 5,998 pia inajulikana kama LR 14207 inayomilikiwa na Amaka Development Limited., mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Sagalla Ranch: hekta 17,402 pia inajulikana kama LR 12177 inayomilikiwa na Sagalla Ranchers Limited, mkusanyiko wa wanahisa wazawa.
- Ndara Ranch: hekta 1,834.77 pia inajulikana kama LR 12176 inayomilikiwa na Eliud Timothy Mwamunga, mdau wa ndani.
- Choke Ranch: hekta 5,076 pia inajulikana kama LR 12199/3 inayomilikiwa na Raymond Joel Mwangola mdau wa ndani.

- Kutima Ranch: hekta 5,076 pia inajulikana kama LR 12199/4 inayomilikiwa na Kutima Investments Limited, mkusanyiko wa wanahisa wazawa.

Ranchi hizi za Kikundi ni sehemu ya ardhi inayounda ukanda kati ya Hifadhi ya taifa ya Tsavo Mashariki na hifadhi ya Taifa ya Tsavo Magharibi. Ukanda huu unafika hadi safu ya mwisho ya milima ya Marungu. Eneo la mradi na eneo lisilo ndani ya mradi limeweka katika nyaraka Kielelezo 1, na mipaka yote zimepatikana katika vitabu za mkaguzi wa mradi. Ardhi iliyoko ndani ya mradi imeainishwa kuwa eneo lenyo misitu mikavu ya kitropiki kwa angalau miaka 20 na imekuwa misitu ambayo haijaguswa katika historia ya eneo hilo.

Madhumuni ya mradi huo ni kulinda milele misitu ya nchi kavu inayounda eneo la mradi na ambayo inaunda ukanda wa mtawanyiko na uhamiaji wa wanyamapori kati ya Mbuga za Kitaifa za Tsavo Mashariki na Tsavo Magharibi, ili kuhifadhi bioanuwai muhimu inayopatikana katika misitu hiyo, ili kutoa njia mbadala. fursa za maendeleo endelevu kwa jamii za wenyeji zinazoishi karibu na misitu na kuzuia Uzalishaji wa hewa ukaa ambao ungetokea ni zile misitu ya nchi kavu kugeuzwa kuwa kilimo cha kujikimu kwa kutumia mbinu za Kufyeka na Kuchoma kawaida kwa eneo hili la Kenya.

Lengo kuu la Shughuli za mradi ni kuanzisha miradi endelevu ili kuboresha maisha ya wananchi wa eneo hilo, hii imeweza kuafikiwa kupitia ajira ya moja kwa moja na pia kupitia miradi iliyoanzishwa ili kuzalisha mapato. Kwa wastani, Wildlife Works imeweza kutoa ajira kwa watu kati ya 292-331 kutoka katika eneo la mradi. Mbali na shughuli za msingi za mradi, mapato kutokana na mauzo ya hewa kaa kupitia Wildlife Works Carbon Trust (WWCT) yameweza kufaulisha miradi endelevu kwa jamii

KCRPII hutoa faida nyingi ambazo zitasaidia Kenya kuafikia malengo ya maendeleo endelevu ya ulimwengu (SDGs). Mwaka 2015, Kenya ilijiunga na jumuiya ya kimataifa katika kupitisha malengo yake ya SDGs, ambayo ni seti ya malengo 17 ya ulimwengu wote yanayolenga kuangaza mazingira, uchumi na jamii. Mfumo huu umetengenezwa kusaidia kukusanya fedha na kuhakikisha kuna mipangilio ya kuboresha maisha ya wanadamu. Mwaka 2016, Kenya ilitekeleza mpango wa Dira ya maendeleo ya mwaka 2030, mpango wa maendeleo wa muda mrefu kwa lengo la kuigeuza Kenya kuwa nchi mpya ya viwanda na ya kipato cha kati ambayo inatoa maisha bora kwa raia wake wote ifikapo mwaka 2030. Hii yote itafanyika kupitia mfumo bora unao zingatia mazingira bora kwa wote.

Mipango hii miwili ya maendeleo endelevu inaratibiwa katika malengo yao na maeneo muhimu ya mradi. Mradi wa KCRPII unachangia nchi hii kuafikia malengo haya. Wildlife Works itatumia mfumo uliowekwa na kanunua za kufwatilia mradi wa CCB & SD VISta. SDGs ambazo KCRPII itachangia moja kwa moja katika ratiba zao.


- Lengo la kwanza: Kupunguza umaskini.
- Lengo la pili: Kuangamiza njaa.
- Lengo la tatu: Afya bora kwa wote.
- Lengo la nne: Elimu bora.
- Lengo la tano: Usawa wa Jinsia zote.
- Lengo la sita: Maji safi na salama kwa wote.
- Lengo la nane: Kazi na uchumi bora.
- Lengo la kumi: Kupuguza ukosefu wa usawa.
- Lengo la kumi na mbili: Matumizi Endelevu na Mifumo ya uzalishaji.
- Lengo la kumi na tatu: hatua za kuangazia mazingira bora.

- Lengo la kumi na tano: Maisha mema duniani.
- Lengo la kumi na sita: Amani na umoja kwa maendeleo endelevu, Upatikanaji wa Haki kwa Wote, Ufanisi, Uwajibikaji, na Taasisi Jumuishi katika ngazi zote.
- Lengo la kumi na saba: Kuimarisha Njia za Utekelezaji na Kufufua Ushirikiano wa Kimataifa wa Maendeleo Endelevu.

Faida zinazotokana na mazingira bora ni kuhakikisha misitu iliyoko katika maeneo ya mradi imeweza kuhifadhi tani of 14,883,342 kwa ujumla za hewa chafu ya carbon wakati wa kipindi hiki cha ufuatiliaji na ukaguzi wa mradi Mradi huo utazalisha faida kubwa za jamii na viumbe hai. Fursa mpya za kuanzisha miradi endelevu zitawekwa, kama vile ajira ya moja kwa moja, shughuli mbadala za kuzalisha mapato (IGAs) na mipango ya kuchochea uwekezaji katika biashara zitaundwa ili kupunguza shinikizo kwa mazingira wakati wa kuongeza ustawi wa jamii. Miradi za ziada zitashughulikia usalama wa chakula, kuboresha vituo vya afya na elimu, pamoja na kuongeza elimu ya mazingira. Uhifadhi wa misitu na wanyama pori pia utachangia pakubwa kuhakikisha mradi unaendelea. Mradi huu pia unalinda makazi muhimu ya spishi nyingi zilizoorodheshwa na IUCN kuwa ziko hatarini kupotea, ikiwa ni tembo, zebra aina Grevi, Simba, Mbwa mwitu, chui, duma, Ndege aina ya Sekretari, ndege aina ya Martial Eagle, ndege aina ya Bateleur na aina kadhaa za volcha.

Tafadhali tembelea tovuti ya usajili ya VERRA - https://registry.verra.org/app/projectDetail/VCS/612, au Ofisi ya Mradi iliupate nyaraka kamili za mradi.

Eneo la mradi.




Kielelezo cha 1: KCRPII Eneo la mradi

| Extent Boundary | Location (Easting, Northing UTM Zone 37S) |
|---|---|
| Northern Extent GPS Point | 458240 E, 9619262 S |
| Eastern Extent GPS Point | 503214 E, 9584109 S |
| Southern Extent GPS Point | 465903 E, 9552171 S |
| Western Extent GPS Point | 422023 E, 9598523 S |

## Tarehe muhimu za Mradi na yaliyoafikiwa.

| Tarehe | Yaliyoafikiwa katika Maendeleo na Utekelezaji wa Mradi. |
|---|---|
| 01 Januari 2010 | Tarehe ya kuanza kwa mradi |
| 01 Januari 2010 | Kuanza kwa shughuli za Mradi, ulinzi wa misitu kutokana na ukataji miti na uharibifu, Tarehe ya Kuanza kwa Mradi, |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa | Mradi wa kukuza Jojoba. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa | Mradi wa greenhouse na maeneo ya kuuza miche unaofaulishwa na Wildlife Works. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa. | Upanzi na uhafadhi miti mlima Kasigau na maeneo Jirani. |
| Kuanzia mradi uanze(2010) – hadi sasa. | Uundaji na uboreshaji wa mashule na maeneo ya kusomea, miundo misingi, kufadhili masomo ya wanafunzi kwa kuwalipia karo, kuanzisha na kuboresha kilimo-biashara, maji safi na afya bora kwa wote. |
| Kuanzia mradi uanze(2010) – hadi sasa. | Kitengo cha maaskari wa Wildlife Works wanaolinda misitu na Wanyama pori. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa. | Ufuatiliaji wa misitu na bionuawai. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa | Uuzaji wa bidhaa zinazotoka/kuzalishwa kutoka kwa eneo la mradi. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa | Patroli na kulinda usalama wa maeneo ya misitu unaofanywa na askari pori. |
| Kuanzia mradi uanze (2010) – hadi sasa | Ufuatiliaji wa hela ya aina ya carbon inayotoka katika misitu eneo la mradi. |


| | |
|---|---|
| Upanuzi uliokamilika Oktoba 2011 | |
| Kiwanda cha kutengeneza nguo kilifunguliwa mwaka wa 2011 | Upanuzi wa kiwanda cha kushona nguo. |
| 27 Aprili 2011 | Uhakiki na ukaguzi na wa mradi kupitia mfumo CCB. |
| 13 Mai 2011 | Uhakiki na ukaguzi wa mradi kupitia VCS. |
| 13 Mai 2011 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo VCS M1 |
| 25 Mai 2011 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa CCB M1 |
| Ilijengwa 2012 na kuhifhadi bora hadi leo. | Kuboresha na ujenzi wa ofisi za renchi. |
| 30 Novemba 2012 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupita mfumo wa VCS M2 |
| 05 Disemba 2012 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa CCB M2 |
| 2012 – hadi sasa. | Msaada kwa Mashirika ya Msingi ya Jamii: Sagalla Conservation and development forum (SCADF), Mwatate District stakeholders forum (MDSF), Mwachabo Development Forum (MDF), Marungu Hills Conservancy Association (MHCA), Kasigau Development Trust (KDT) na Mackinnon Road CBO. |
| Ilianza katika awamu ya kwanza ya mradi 2011, ilihamia kituo kipya kilichoko Taita Ranch mapema 2013 – Hadi sasa. | Eneo la kutengenezea makaa zingira inayofadhiliwa na Wildlife Works. |
| Jengo mpya linalofanyiwa | Mradi wa kutengeneza sabuni inayofadhiliwa na Wildlife Works. |

| | |
|---|---|
| kazi kuanzi 2013 hadi sasa. | |
| 21 Mai 2013 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa VCS/CCB M3 |
| 2013 – hadi sasa | Kiwanda cha kutengeneza nguo zinazouzwa nchini. |
| 2013 – Miradi kadhaa ilitatizwa na Uviko-19. | Miradi za kiafya zanazotekelezwa na Wildlife Works. |
| 2014 – hadi sasa | Msaada wa kuhakikisha Tsavo Conservancy inaanzwa. |
| 02 Septemba 2015 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa CCB/VCS M4 |
| 24 Agosti 2018 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo CCB/VCS M5 |
| Ilianzishwa rasmi 2019 – hadi sasa | Miradi za kuboresha na kukuza utalii kama vile kujengwa kwa hoteli ya Kivuko. |
| 12 Juni 2020 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa CCB/VCS M6 |
| 06 Desemba 2021 | Uthibijitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa CCB/VCS M7 |
| 16 Mai 2022 | Mradi na tarehe iliyowasilishwa kwa orodha ya mpango na kutumia mfumo wa ukaguzi wa SD VISta na Verra. |
| 22 Juni 2022 | Uthibitishaji na ukaguzi wa mradi kupitia mfumo wa wa VCS / CCB M8, na uthibitishaji wa SD VISta na ukaguzi wa mradi. |

## Maeneo muhimu yanayoangaziwa ya jamii.


**Swala muhimu ya la kwanza la kuangaziwa. Utawala, uongozi na ujumuishaji wa jinsia zote kwa maswala yajamii.**

Kama kuna elimu endelevu na wanajamii ambao wako na tajriba ya kuelewa na kusuluhisha maswala muhimu ya jamii, kama kuna viongozi wenye uwezo wa kutoa uongozi bora na kujenga taasisi imara, na kama utawala wa sheria utalindwa, basi tutakuwa na utawala bora.





**Swala la pili muhimu la kuangaziwa: Umaskini: Kutenenza Ajira na shughuli za kuzalisha kipato.**

Ikiwa tuna jamii yenye ujuzi, na ikiwa usimamizi bora wa mazingira unasaidia shughuli mbalimbali za kuzalisha mapato na kuhakikisha usalama wa chakula kwa kaya zote, basi umaskini utapunguzwa.




**Swala la tatu muhimu la kuangaziwa: Mkwaruzano kati ya Wanyama pori na binadamu.**

Ikiwa kuna uvunaji wa maji na makazi ya wanyamapori imelidwa ipaswavyo, ikiwa Wanyama pori walisimamiwa vizuri na kudhibitiwa ndani ya makazi yao, na ikiwa usalama wa chakula ulihakikishiwa na mapato kuongezeka, basi migogoro ya binadamu na wanyamapori itapunguzwa.





**Swala la nne muhimu la kuangaziwa: Uharibifu wa mazingira: ikiwa ni pamoja na ukataji miti na masuala ya kilimo.**

Ikiwa jamii itatekeleza mbinu bora za kilimo, kama upandaji wa miti unafanywa katika maeneo ya kilimo na misitu, na kama umiliki wa ardhi utaangaziwa, basi uharibifu wa mazingira utapungua na miti kuongezeka na kusababisha mazingira mazuri.



**Swala la tano lakuangaziwa: Elimu.**

Kama jamii itangazia elimu kwa kina, kama kuna fedha kwa ajili ya sekta ya elimu kutoka kwa serikali na wafadhili wengine, na kama rasilimali zote za elimu zitatumika vizuri, basi tutafikia viwango vya juu vya elimu.




Kielelezo cha 2: Matokeo yanaelezea mabadiliko kwa masuala matatu yaliyotambuliwa na wanajamii wa mradi kupitia warsha iliyoandaliwa katika eneo na mradi.